



**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA CHUO CHA UANDISHI
WA HABARI NA MAWASILIANO NAM. 11 YA 2006**

MPANGILIO WA VIFUNGU

VIFUNGU

MAELEZO

**SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.


**SEHEMU YA PILI
MASHARTI YA KUFUTA NA KUBAKIZA**

3. Kufuta na Kubakiza.



SHERIA NAM. 13 YA 2020

NIMESAINI



{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI

29 Januari,....., 2020

**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA CHUO CHA UANDISHI
WA HABARI NA MAWASILIANO NAM. 11 YA 2006**

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

**SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI**

Jina fupi
na kuanza
kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Kufuta Sheria ya Chuo cha Uandishi wa Habari na Mawasiliano Zanzibar Nam. 11 ya 2006, na itanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saina na Rais.

Ufafanuzi.

2. Katika Sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo:

“Chuo” maana yake ni Chuo cha Uandishi wa Habari na Mawasiliano Zanzibar;

“Rais” maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

“Sheria iliyofutwa” maana yake ni Sheria ya Chuo cha Uandishi wa Habari na Mawasiliano Nam. 11 ya 2006.

**SEHEMU YA PILI
MASHARTI YA KUFUTA NA KUBAKIZA**

Kufuta na
Kubakiza.

3.-(1) Sheria ya Chuo cha Uandishi wa Habari na Mawasiliano Nam. 11 ya 2006 inafutwa.



(2) Bila ya kujali masharti ya kufuta chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki:

- (a) teuzi, kanuni, amri au mambo mengine yoyote yaliyotekelezwa au kufanywa chini ya Sheria iliyofutwa kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii yataendelea kuwepo na kufanya kazi hadi pale yatakaporekebishwa, kufutwa au kubadilishwa chini ya masharti ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Nam. 8 ya 1999;
- (b) wanafunzi wote waliodahiliwa kwa mujibu wa kanuni za udahili za Chuo zilizotungwa chini ya Sheria iliyofutwa wataendelea kukamilisha mafunzo yao na kutunukiwa vyeti kwa jina la Chuo kulingana na Sheria iliyofutwa na kanuni zake; na
- (c) watumishi waliopo hivi sasa wa Chuo wataendelea kutekeleza majukumu yao chini ya masharti ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Nam. 8 ya 1999 na Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

UMEPITISHWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 18 Juni, 2020.

.....
(RAYA ISSA MSELLEM)

Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.